

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI**

**07 JUNI, 2023**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

---

### **MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 07 JUNI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **544. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara za Vijijini zinazopita katika vilima vikali.

##### **545. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaupa hadhi ya Manispaa Mji wa Kibaha ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani.

##### **546. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Kwamagome.

**547. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN  
KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inachukua hatua gani kupata Viwanja vya Michezo na kuvilinda kwani baadhi ya Shule zimetumia kujenga Madarasa.

**548. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO  
(MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja Mto Mnyamansi ili Barabara ya Kambanga - Ifinsi hadi Bungwe iweze kutumika.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**549. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA  
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Benki ya CRDB itafungua Tawi katika Mji wa Mangaka.

**550. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu ucheleweshaji fedha zinazotumwa Nje ya Nchi kutokana na Mabenki kuwa na uhaba wa fedha za Kigeni.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**551. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa kutambua *fire hydrants* nchini na kuziwekea alama ili kusaidia wakati wa majanga ya moto.

**WIZARA YA NISHATI:**

**552. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Wananchi waliopitiwa na ujenzi wa Bwawa la umeme la Mto Lumakali Makete watalipwa fidia.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**553. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ubunifu una nafasi gani katika kuleta mageuzi ya kiuchumi.

**WIZARA YA AFYA:**

**554. MHESHIMIWA BERNADETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**555. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya Wananchi wa Kata ya Tambukareli na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **556. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali italeta Mradi wa Kuhifadhi Mazingira katika chanzo cha maji cha Mto Ruaha na Shamba la Miti la Sao Hill.

### **557. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mabwawa katika Mito Ghona, Rau na Deu ili kupunguza athari za mafuriko.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
07 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**